



Help Me Grow ni mfumo wa kuwasaidia wanawake wajawazito, watoto wadogo na familia kote katika jimbo la Ohio.
Huduma na usaidizi hutolewa kupitia Ziara za Nyumbani na Kuchukua Hatua Mapema.

Swahili



Ziara za Nyumbani (HV) za Help Me Grow ni mpango wa kujitolea wa nyumbani unaotolewa kwa familia yako bila malipo. Wahudumu wetu wa kuzuru nyumbani ni wataalamu wenyewe ujuzi ambao hutumia njia ya ukarimu kutoa maelezo na usaidizi wakati wa ujauzito, na kukuwezesha wewe kama mzazi kwa kukupa ujuzi, zana, na ujasiri wa kumlea mtoto wako awe na afya bora katika miaka yake ya kwanza - ambayo ni kipindi muhimu cha ukuaji wake.

NI NANI ANAYEPSWA KUPENDEKEZWA?

Wanawake wajawazito na familia zilizo na watoto wachanga.

NI NINI UNACHOWEZA KUTARAJIA?

Familia yako itakapopendekeza, utapewa mtaalamu wa kuzuru nyumbani. Mhudumu wa kuzuru nyumbani wa Help Me Grow atakupa usaidizi wa utunzaji na maelezo ya kuaminika kuhusu mada ambazo ni muhimu zaidi kwako kuhusu ujauzito na ukuaji wa mtoto wako. Iwe ni hatua unayoweza kuchukua ili uhakikisha umekuwa na ujauzito mzuri, jinsi ya kumtuliza mtoto wako anayelia, jinsi ya kudhibiti usingizi wake (na wako pia!) au jinsi ya kukabiliana na matatizo ya uzazi, mtaalamu wako anayezuru nyumbani atakusaidia, kukusikiliza na kukuunganisha na wahudumu wa jamii kulingana na mahitaji yako. Sisi tunakuwezesha kufanya maamuzi ya kibinasi kuhusu mambo yanayokufaa wewe na mtoto wako.

MANUFAA YA ZIARA ZA NYUMBANI:


Matokeo bora ya kujifungua - wanawake wajawazito ambao walishiriki katika HV walikuwa na asilimia 48 ya watoto wanaozaliwa wakiwa na uzito mdogo.

Kuungeza Utayari wa Kuhudhuria Shule kwa Watoto - Watoto walioshiriki katika HV walikuwa na alama zaidi kwa asilimia 25 katika darasa la kwanza hadi la tatu katika mitihani ya mafanikio ya kusoma na hisabati.



Je, una ujauzito au
unamlea mtoto
mdogo?

Ili upate maelezo zaidi kuhusu mipango hii au ujisajili,
unaweza: Piga simu 1-800-755-GROW
Tembelea www.helpmegrow.org



Help Me Grow Early Intervention (EI) huzisaidia familia zenye watoto wadogo ikiwa kuna hali za ulemavu na kucheleva kukua. Huduma za EI kawaida hutolewa nyumbani mwako au maeneo mengine ambapo familia yako huzuru, na hujenga uwezo wako wa kuimarisha kujifunza na kukua kwa mtoto wako.

NI NANI ANAYEPSWA KUPENDEKEZWA?

Watoto kutoka kuzaliwa hadi umri wa miaka mitatu wakati kuna wasiiasi kuhusu ukuaji wao au utambuzi wa kimatibabu wa hali ambayo inaweza kuathiri ukuaji.

NI NINI UNACHOWEZA KUTARAJIA?

Baada ya kupendelekeza, wahudumu wa mpango wa EI wa eneo lako watateua mratibu wa huduma kwa familia yako. Mratibu wako wa huduma atakuwa mwasiliani wako wa msingi wa EI na ataisaidia familia yako kwenye hatua zako zote katika EI. Ikiwa mtoto wako anastahiki kufanyiwa EI, mratibu wako wa huduma atakuomba umpe idhini ya kukamilisha tathmini ya mtoto na familia. Timu yako ya EI itapata maelezo zaidi kuhusu maslahi na uwezo wa mtoto wako na vipaumbele na shughuli za kawaida za familia yako. Watatumia maelezo haya ili kuweka matokeo lengwa ambayo ungependa kufikia. Matokeo haya yatakuwa sehemu ya Mpango wa Huduma ya Familia kwa Mtu binafsi (IFSP). Matokeo ya IFSP yako yataandikwa kwa msingi wa kile unachotaka mtoto au familia yako iweze kufanya katika shughuli za kawaida za familia yako. Wanatumia maneno yako mwenyewe na kuzingatia mambo muhimu kwa familia yako. IFSP pia inaelezea huduma moja au kadhaa zitakazohitajika kukusaidia kufikia matokeo lengwa.

MANUFAA YA KUCHUKUA HATUA MAPEMA:

Katika miaka ya hivi majuzi, zaidi ya asilimia 95 ya wazazi wa Ohio ambao watoto wao walihudumiwa katika EI waliripoti kuwa walipata uwezo zaidi wa kumsaidia mtoto wao kujifunza mambo mapya na kupata stadi mpya. Idadi hiyo hiyo iliripoti kuwa EI iliwasaidia kuwasiliana na watu wengine kuhusu mahitaji ya watoto wao.



Je, una wasiiasi
kuhusu ukuaji wa
mtoto wako?